BARUA YA WAZI KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, JOHN JOSEPH POMBE MAGUFULI KUHUSU AFYA KWA WOTE

Mheshimiwa mpendwa Rais wetu,

Mheshimiwa Rais, kwanza kabisa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Health Promotion na wafanyakazi wake wote, naomba nikupongeze kwa uongozi wako kwa kuiongoza Tanzania katika kipindi kigumu ulipoikuta. Umeifanya nchi yetu ijulikane na kila nchi hapa duniani hata zile ambazo zamani waliuliza Tanzania ni wapi na Rais wake ni nani? Siku hizi jina lako na Tanzania limekua maarufu kushinda almasi. Baadhi ya yale ambayo yalikuwa yanaonekana kama hayawezekani, kwenye uongozi wako sasa yanawezekana. HONGERA SANA!

Tunalazimika kukuandikia barua ya wazi kuelekea siku ya afya duniani baada ya kuona hii ni njia rahisi na mbadala ya kuwasiliana nawe ingawa yaliyomo kwenye barua hii tungependa tuyawasilishe ana kwa ana.

Mheshimiwa Rais, sera ya afya ya nchi ya Tanzania inatamka bayana kwamba afya ya msingi itawafikia Watanzania wote kwa kiwango kilicho bora na bila kujali hali ya mtu. Mkakati wa afya wa nne unaahidi kuzifikia kaya zote kwa huduma bora za afya. Dunia yote sasa imeazimia kuwapatia watu wote huduma za afya na malipo yasiwe kikwazo (Universal Health Access). Ili kukidhi hitaji hilo, Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia zimependekeza kila nchi itenge kiwango cha asilimia 4-5% ya pato la Taifa kwa ajili ya sekta ya afya.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya duniani, Serikali ya Tanzania ilitumia asilimia 1.3% mwaka 2015 na ulipoingia madarakani ukaipandisha kuwa 1.7% ya Pato la Taifa kwenye afya. Ijapokuwa hii inafariji sana, lakini ni chini ya kiwango pendekezwa ili kuwafikia wanyonge wasioenda hospitalini kwa sababu hawana fedha.

Huduma za afya kwa wote ni ajenda ya Urais na tunaweza kujifunza kutoka nchi nyingine. Mwaka 2006 Rais wa China, Hu Jintao alibeba ajenda ya Universal Health Coverage mwenyewe na ilipofika mwaka 2011 asilimia 95% ya Wachina walikuwa na bima za afya. Waziri Mkuu wa Thailand Mh. Thaksin mwaka 2002 alianzisha ajenda ya huduma za afya kwa watu wote na akafanikiwa. Rais wa Indonesia, Mh. Jokowi mwaka 2014 alianzisha ajenda ya huduma bora za afya kwa watu wote na akafanikiwa. Aliyekuwa Rais wa Marekani, Barack Obama mwaka 2012 alianzisha mpango wa huduma za afya kwa wote uliojulikana kama Obama Care. Rais wa Rwanda, Mh. Paul Kagame alianzisha ajenda ya huduma za afya kwa watu wote na ilipofika mwaka 2011, asilimia 91% ya Wanyarwanda walikuwa na bima. Rais wa Kenya, Mh. Uhuru Kenyatta amebeba ajenda ya huduma za afya kwa watu wote (Universal Health Coverage) kuwa kati ya ajenda nne za uongozi wake.

Mheshimiwa Rais, mkakati wa kutafuta rasilimali za sekta ya afya ulilenga kutoa mwongozo wa namna ya kuweka bima inayochangiwa na Serikali ili kumfikia kila Mtanzania na kupunguza kabisa malipo ya papo kwa papo (out of pocket) kwa bahati mbaya sana, mkakati huu bado haujaidhinishwa na Serikali yako toka mwaka 2015. Hali hii inazuia uundwaji wa fungu la kitaifa la fedha ambalo lingemsaidia kila Mtanzania na hasa Mtanzania mnyonge kupata huduma za afya. Kutokana na hali hiyo, Wizara ya Afya ilikadiria mwanzoni mwa mwaka huu wa fedha (2018/19) kuwa karibu asilimia 66% ya Watanzania hawana Bima ya Afya ya aina yoyote ile. Hii imepelekea karibu kumi katika mia wanatumia asilimia 10 ya kipato cha mwaka kwa huduma za afya, hiki ni kiwango kidogo ukilinganisha na Rwanda ambayo ni chini ya asilimia tano.

Mheshimiwa Rais, kutoa huduma za afya kwa kila Mtanzania ni mkakati muhimu kwa Serikali yako katika kuyafikia malengo ya Sustainable Development Goals (SDGs). Hii ni ajenda muhimu na ni mkakati muhimu kwako Mheshimiwa Rais ili kufikia Tanzania ya Viwanda. Kama vile Marais hapo juu walivyoichukua ajenda ya Huduma za afya kwa watu wote (Universal Health Coverage).

Mheshimiwa Rais, Afya kwa Wote ina manufaa katika nyanja tatu muhimu: kiafya, kisiasa na kiuchumi: Ni njia mojawapo ambayo itakuonyesha kwamba unawajali wananchi wako wanyonge.

Utafiti uliofanywa na watafiti mahiri duniani unaonyesha kwamba mpango wa afya kwa wote unaboresha viashiria vya afya bora ya wananchi walio wengi. Katika Jarida Maalum la Lancet, watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Imperial College London kutoka zaidi ya nchi 150 duniani waliona kwamba: "kutoa huduma za afya kwa wote hupelekea matumizi ya fedha za Serikali kupunguza fedha zinazopunguza vifo vya watoto na akina Mama."

Mheshimiwa Rais, mpango wa huduma za afya kwa wote una faida za kisiasa, kiuchumi na kiafya:

Kisiasa: Kila Mtanzania atakumbuka wakati ambao aliumwa na kwenda kutibiwa hospitali hata pale ambapo alikuwa hana fedha na hapo ndipo ataikumbuka Serikali yako jinsi ilivyo mtendea. Kwa hiyo viongozi wa kisiasa ni vizuri kuwekeza katika afya kwa wote kama mtaji wa kisiasa. Wanasiasa walio wengi duniani hujipatia umaarufu wanapowekeza katika sekta ya afya. Watanzania walio wengi huenda kwa waganga wa kienyeji, sio kwa sababu wanapenda bali kwa kuwa hawana jinsi ya kwenda kutibiwa hospitalini. Mwaka 2004 mwanzilishi wa Afya kwa Wote kutoka Canada, Tommy Douglas alipigiwa kura kama ***Shujaa wa Mageuzi ya Afya kwa Wote*** nchini Canada. Tunakuomba uichukue ajenda hii kwa manufaa ya taifa la Tanzania na mageuzi ya kisiasa.

Kiuchumi: Familia ambazo zinafaidika na Afya Kwa Wote huwa na afya bora na huwa na kipato kizuri kwa vile hawahitaji kuweka fedha za akiba kwa ajili ya matibabu ya siku za mbele. Fedha zao zinatumika katika kuwekeza na mahitaji mengine muhimu ya kifamilia. Na hali hii inaenda sambamba na dira yako ya kiuchumi na uchumi wa nchi ya Viwanda. China iliamua kwa makusudi kabisa kuongeza fedha kwa ajili ya huduma za afya ili kuhakikisha kwamba wananchi wake wanapunguza kuwekeza katika maeneo ambayo sio muhimu, matokeo yake ni kwamba China ni nchi ya pili kwa uchumi mkubwa duniani ikitanguliwa na Marekani.

Kiafya: Kuwekeza kwenye mpango wa afya kwa wote kunachangia kufikia malengo ya maendeleo endelevu (Sustainable Development Goals). Uchambuzi umeonyesha kuwa kuwekeza kwenye mpango wa huduma za afya kwa wote kutachangia Tanzania kufikia SDG1 (Poverty Reduction), SDG3 (Equitable Sustainable Health), SDG4 (Quality Education), SDG5 (Gender Equity), SDG6 (Inclusive societies) na SDG8 (Inclusive economic growth).

Mheshimiwa Rais, tumekuchosha na maneno mengi. Tunaomba radhi kwa hilo. Tunakuomba yafuatayo:

1. Uibebe ajenda ya afya kwa kila Mtanzania (Universal Health Coverage) kama ajenda ya kipaumbele kwenye vipaumbele vyako. Hivyo uitishe wadau na kuwaambia azma yako kuhakikisha kuwa hakuna Mtanzania atakosa huduma kwa sababu hana fedha (Leave No One behind),
2. Uidhinishe na kutekeleza mpango wa Afya kwa Wote na kuweka mfumo wa kisheria wa kuhakikisha kwamba kuna mfumo mmoja wa Bima ya Afya ambao utazuia watu kulipia huduma za afya kutoka mifukoni mwao na ambao fedha zake zitatoka serikalini,
3. Serikali iamue kutafuta fedha kwenye kodi maalum kwa ajili ya huduma za afya kwa watu wote ikiwa ni pamoja na wenye uwezo kulipia zaidi kwa ajili ya wanyonge na Serikali kuongezea fedha kwa ajili ya wanyonge pia (Subsdize),
4. Serikali ianze kuongeza mchango wa fedha zake za ndani kwenye huduma za afya kufikia asilimia 4-5 ya pato lake ifikapo mwaka 2030,
5. Itungwe sheria na kurekebisha zilizopo ili kuruhusu utoaji wa huduma za afya na bima hapa nchini ili kuwe na bima ya afya moja tu, na kwamba fedha zote zitaelekezwa kwenye mfuko mmoja wa bima.

Mwisho kabisa, Mheshimiwa Rais ukichukua ajenda hii na kuifanikisha, nchi yetu itakuwa kati ya nchi bora duniani zinazojali wananchi wake na kukuza uchumi na itakuwa rahisi kwa sababu jamii ni yenye afya. Tumalize kwa kauli mbiu ya mpango huu....."LEAVE NO ONE BEHIND" Tusimwache yeyote nyuma.

Mheshimiwa Rais, tunakutakia kazi njema, afya njema na Mungu azidi kukubariki katika kuiongoza nchi yetu.

Wako katika ujenzi wa Taifa,

Rev. Dr. Peter Bujari,MD
Health Promotion Tanzania (HDT)
Email: ed@hdt.or.tz

Tanganyika Farmers' Association Plc

Head Office
P. O. Box 3010, Arusha
Tel: +255 27 254 4872
Web: www.tfa.co.tz
E-mail: tfa@tfa.co.tz

Property Department
P. O. Box 3010, Arusha
Tel: +255 27 254 4298
Web: www.tfa.co.tz
E-mail: property@tfa.co.tz

TAARIFA KWA UMMA

Kampuni ya Tanganyika Farmers' Association (TFA) Plc inachukua nafasi hii kuutarifu Umma wa Watanzania na wadau wote wa kilimo kuwa katika mkutano wake mkuu wa mwaka uliofanyika tarehe 30 Machi 2019 katika viwanja vya "TFA Shopping Centre Arusha", eneo la Ngarenaro pamoja na maazimio mengine wajumbe na wanahisa waliazimia kwa pamoja kuongeza muda kwa Bodi ya Wakurugenzi ya sasa kuendelea kuwepo madarakani kwa kipindi kingine cha miaka mitatu yaani kuanzia tarehe 1 Mei 2019 hadi tarehe 30 Aprili 2022.

Ninachukua fursa hii kuwaomba wadau wetu waendelee kutupatia ushirikiano ili kuendeleza mafanikio ambayo yameanza kuonekana tangu kuchaguliwa kwa Bodi yetu hii.

Pia ninachukua fursa hii kuwapongeza wajumbe wote wa Bodi kwa kuaminiwa na wanahisa wote na kupewa fursa nyingine ya miaka mitatu kuiongoza TFA Plc.

Nawatakia kila la kheri katika kipindi chote cha uongoi katika TFA Plc

Kwa Amri ya Mkutano Mkuu wa Mwaka

Tanganyika Farmers' Association Plc

KATIBU WA KAMPUNI
03/04/2019

Branches:
Moshi, Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, Iringa, Mafinga, Njombe, Mbeya, Mbozi, Babati, Karatu, Mbinga, Makambako, Katesh and Kilolo.

CAN WE DELIVER YOUR PAPER?

YES WE CAN!!!

Just fill the form and call us to collect it from you.

Name/Organisation..... Postal Adress.....
Fax..... Email.....
Contact Person..... Designation.....

I would like to subscribe for

Title	No of Copies	Unit Price
THE CITIZEN		Tsh 1000
MWANANCHI		Tsh 1000
THE EAST AFRICA		Tsh 2000
DAILY NATION		Tsh 1700
BUSINESS DAILY		Tsh 1700

I would like to subscribe for

3 months ☐ 6 months ☐ 12 months ☐

2.5% discount for 3 Months, 5% for 6 Months and 10% for 12 Months

I would like the paper to be delivered to
District.....
Plot /House No.....Street.....
Building.....Floor.....
Room No.....
I will pay by Cheque ☐ Cash ☐ Bank Transfer ☐
Date.....Signature..... Official.....
Stamp.....

To allow us to collect your order from your offices or home residence please call or sms 0754292799 \ 0714532236 or write an email to subscription@the citizenco.tz

THE CITIZEN MWANANCHI MWANA SPOTI